# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

***Dodoma***
***01 Februari, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ameitaka Wizara ya Fedha, Wizara ya Mipango na Uwekezaji, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, kuwezesha na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sera na Mitaala mipya ya Elimu, ili ilete matokeo yaliyokusudiwa katika kuimarisha sekta ya elimu.

Rais Dkt. Samia ametoa tamko hilo leo wakati wa hafla ya uzinduzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la Mwaka 2023 iliyofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Mrisho Kikwete.

Rais Dkt. Samia amesema mabadiliko na kukua kwa kasi kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kunaweza kuwa na mchango chanya au hasi kutokana na namna jamii itakavyojipanga, hivyo ili kuendana na mabadiliko hayo ni lazima kutumia TEHAMA kutoa elimu kwa urahisi na kuwandaa vijana wetu kuwa na taaluma na ujuzi wa taaluma zinazoenda na mageuzi ya TEHAMA bila kuathiri maadili ya vijana hao.

Vile vile, Rais Dkt. Samia amesema Serikali haina budi kuwa na maandalizi ya kutosha kwa kuinua viwango vya ubora wa elimu, na kuwandaa vijana vizuri zaidi ili waweze kumudu stadi muhimu zitakazowawezesha kuajiriwa na kujiajiri pamoja na kuwajengea ujasiri na kuweza kujiamini.

Rais Dkt. Samia pia amesema dhamira ya kufanya mabadiliko katika Sera ni kumuandaa kijana anayejiamini na mwenye nyenzo stahiki za kukabiliana na ushindani wa kikanda na kimataifa ili, kwa kutumia utajiri wa rasilimali zetu, aweze kunufaika kiuchumi

Aidha, Rais Dkt. Samia ameeleza kuwa kupitia Sera ya Elimu iliyoboreshwa, mwanafunzi amalizapo shule ya sekondari, atakuwa na ujuzi na stadi zitakazomuwezesha kutoa mchango kiuchumi kwa jamii inayomzunguka na taifa kwa ujumla.

Sera iliyoboreshwa pia italeta somo la ujasiriamali ambalo litakuwa la lazima kwa kila mwanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne kwa lengo la kumuandaa mwanafunzi kupata misingi ya biashara, ili akiamua kujiajiri kwa kutumia stadi alizopata shuleni, aweze kufanya shughuli zake akiwa na maarifa ya biashara na apate manufaa zaidi.

Vilevile, ili kumuandaa kijana kushindana kikanda na kimataifa, wanafunzi watajifunza lugha mbalimbali za kimataifa ikiwemo kichina, kifaransa na kiarabu ambazo zitawapa umahiri wa lugha, watapata nyenzo muhimu ya mawasiliano na kuwawezesha kufanya biashara kikanda na kimataifa bila kikwazo cha lugha na zitawafungulia fursa mbalimbali zitokanazo na utandawazi.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia amesema Serikali itapitia upya maslahi ya kada ya walimu nchini ili kuipa hadhi inayostahiki kwa kuwa kada hiyo ndio msingi wa taaluma zote, pamoja na kuendelea kuajiri walimu wenye sifa na kuwapa mafunzo stahiki ili waendane na mwelekeo wa Sera mpya.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu